

JIONYESHE MWANAUME
“Umezaliwa wa Kiume, Dhihirisha Uanaume”

WAKFU;

**Naweka Wakfu Kitabu hiki maalum kwa
Mzaliwa Wangu wa kwanza wa kiume Divine-
Chris Elihuruma Maruma, “*Mwanangu eeh,
Umezaliwa wa Kiume, Dhihirisha Uanaume*”.**

SHUKRANI.

Shukrani zangu za dhati ni kwa; -

*i/ Mungu-Mola -YHWH, Kwake ninaishi,
ninatembea na kuwa na uhai.*

*ii/ Mke wangu Kipenzi, Mtoto Mzuri Namwasi
Mathayo Mjema kwa kila kitu.*

*iii/ Mamangu Mzazi Mwl Janeth Kisanga kwa
malezi mazuri yaliyonivusha na mengi.*

*iv/ Watendakazi pamoja nami kwa Huduma ya
Wavulana na Wanaume Katibu Mkuu Nelson
Enock, Waratibu wa Visionary Brothers Ombeni
Jeremiah na Ezra Magalata.*

*v/ CLIMAX Solutions kwa kuchapa kitabu hiki kwa
ustadi mkubwa.*

*vi/ Mdogo wangu na Rafiki wa Faida Elifuraha
Christopher Munisi kwa kuandika kitabu hiki
kwenye Mfumo Kompyuta.*

DIBAJI

Dunia ya leo ina **WANAUME** wachache sana pamoja na kuwa na maelfu ya watu wa jinsia ya kiume. Ni wazi kwamba unaweza kuwa mtu mzima wa kiume lakini bado usiwe **MWANAUME**. Unaweza kuonekana mtu mzima wa kiume lakini ndani yako Wewe ni **MVULANA**.

Hii ni kwa sababu **UANAUME** sio jinsia bali **MAJUKUMU**. Unaweza kabisa kuzaliwa wa kiume, lakini kuwa **MWANAUME** ni mchakato. Zipo hatua, malezi na mafunzo mbalimbali ya kujitambua na kutekeleza ili ufanyike **MWANAUME** kweli kweli. **UANAUME** si kuwa tu na jinsia ya kiume, kuvalaa suruali au mavazi ya kiume, kuongea kwa sauti nzito ya kiume, kuwa kwenye mahusiano na mwanamke au kuitwa jina la kiume, (HAPANA). **UANAUME** ni **MAJUKUMU**, ni kusimama kwenye nafasi na wajibu wako, kama Mungu alivyomkusudia **MWANAUME** awe tangu Adamu.

Kwenye kitabu hiki kidogo nilichowaandikia **WAVULANA**, nimekusudia kutoa mafunzo japo kwa sehemu kidogo ambayo yanalenga kuwaandaa

WAVULANA kuwa WANAUUME. Kwa yeote atakayepata nafasi ya kujisomea kitabu hiki, ipo ari na shauku itainuka ndani yake inayonua kujionyesha kuwa MWANAUME kweli kweli.

Ndani ya kitabu hiki nimegusa mambo mbalimbali muhimu yatakayokusaaidia kuwa MWANAUME, mambo haya ni kama **NI MUNGU ALITAKA, NI MCHAKATO, NI MAJUKUMU, NI UTHUBUTU, NI UWAKILI, NI UBABA** na mengine mengi. Mambo haya muhimu yapo takribani ishirini (20), yatajenga msingi mzuri kwako wa kufanyika na kujionyesha MWANAUME KWELI KWELI!

**Umezaliwa wa Kiume, Dhihirisha Uanaume!
Brother Elihuruma Maruma
Januari, 2019**

1. Ni MUNGU alitaka!

“Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujuua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa.” Yeremia 1:5

“La Sivyo, Ee binadamu; wewe u nani umjibuye Mungu?! Je! Kitu kilichoumbwa kimwambie yeye aliyekiumba, Kwani kuniumba hivi?”. Warumi 9:20

Naamini Wewe unayesoma kitabu hiki sasa ni wa kiume, basi ninayo habari njema kwako ambayo inawezekana uliwahi kuisikia, ila sio kwa umaalumu kama hivi. Najua unajua kwamba Muumbaji wa vitu vyote ni Mungu ukijumuisha na wewe, sasa pokea taarifa hii kwamba MUNGU ndiye ALIYETAKA na aliyekusudia WEWE kuzaliwa wa kiume. Na tena hakufanya kwa kubahatisha, kimsingi kazi au jukumu (KUSUDI) alilokuleta kufanya duniani, ndilo linaloendana na Wewe kuwa wa KIUME. Tena hii ndio sababu kubwa Wewe kuzaliwa wa kiume.

Lakini pia MUONEKANO wako na jinsi ulivyo kwa ujumla, ndio hasa Mungu alitaka uonekane hivyo ili

uweze kufanya kwa urahisi, ustadi na ufanisi kila alilokuumbia kufanya. Kwa hiyo kaka, hebu jikubali, jipende na jithamini namna ulivyo na mshukuru sana Mungu kukuumba wa kiume aisee. Unajua wakati unafanyika tumboni Mungu alihusika kwa 100% kuhakikisha unatoka kama alivyotaka utoke.

Haitoshi na huku duniani nako wakati unazaliwa, wakakuangalia wakaona wewe ni wa kiume, walifurahishwa sana na ujio wako. Na ndani ya mioyo na fikra zao waliona mtoto wa kiume ambaye atafanyika MWANAUME, KIONGOZI, MUME na BABA kwa siku zijazo. Walitegemea hayo kwa moyo na kwa tumaini kubwa, Familia, Jamii, Kanisa na Taifa lilitegemea kupata MWANAUME, atakayekuwa Nguzo na Mhimili wake katika kuleta maendeleo na maboresho, Na wala sio balaa na majanga.

Na Mungu alivyo wa ajabu, Nampenda sana, Alishaweka ndani yako kila unachohitaji ili kuliishi kusudi lake inavyopaswa. Ndani yako aliweka UANAUME, UONGOZI, UBABA na kila unachohitaji sawasawa na majira na nyakati. Na tena hata siku zako za kuishi alishaziandika zote, na

yakupasayo kufanya kwa kila siku. Tambua haukuzaliwa kama ajali, au kwa bahati mbaya au eti kwa majaribio, HAPANA, ulizaliwa kuja kuwa majibu kwa watu wengine, suluhisho la matatizo, na upenyo kwa changamoto. Wewe ni mtu wa maana sana hapa duniani.

Hauna sababu ya kuishi kwa woga, wasiwasi, kutojiamini au kuchanganyikiwa. Mungu ni sababu ya Wewe kuzaliwa wa kiume, na ni sababu ya wewe kupata wasaa na fursa ya kuishi hata leo. Hebu chagua kumtii, kumpenda, kumheshimu, kumwabudu na kumtegemea kwa kila hatua, na utamwona akinyoosha mapito yako. Narudia, Mungu alitaka Wewe uzaliwe wa kiume, na ndio maana wewe sio wa kike ahahahahahahah....

2. Ni UFAHAMU!

*“Ufahamu ni chemchemi ya uzima kwake aliye nao;
Bali kufundishwa kwa wapumbavu ni upuzi wao”*
Mithali 16:22

*“Hekima huwa machoni pake mwenye Ufahamu;
Bali macho ya mpumbavu huwa katika ncha za
dunia.”* **Mithali 17:24**

Kwa kukosa ufahamu sahihi juu ya UANAUME, leo dunia ina upungufu mkubwa sana wa WANAUME. Biblia inasema UFAHAMU ni chemicheni lakini pia huchochea hekima, Hekima humwezesha mtu kuishi kwa usahihi kama inavyotakikana. Hatari tuliyonayo leo, Watu wengi wamezaliwa wa kiume lakini wamekosa UFAHAMU juu ya UANAUME. Lakini wangeliipata Ufahamu sahihi juu ya Uanaume kama alivyokusudia Mungu, wangeliishi kwa hekima za kiume na wangefanyika Wanaume halisi.

Japo nimeongelea kwa undani kidogo kwenye MAJUKUMU ya Uanaume, acha nikukumbushe hapa kwamba kila mtu aliyezaliwa wa kiume na kuitwa mvulana, anatarajiwa kuwa MWANAUME,

KIONGOZI, MUME pia BABA. Na hii sio kwa majina tu bali kwa majukumu halisi. Mwanaume yeote amebeba UTAMBULISHO, URITHI na HATIMA ya jamii, kanisa na taifa.

Moja kati ya misingi imara ya kufanikiwa kwa mtu ni KUJITAMBUA. Na katika kujitambua huku ni vema ukajua kwa undani uwezo na udhaifu wako, lakini pia fursa na hatari ulizonazo ie **SWOT**- Strengths, Weaknesses, Opportunities, na Threats.

Ngoja nikudokeze kidogo juu ya MWANAUME alivyo, halafu hayo mengine utaendelea kujitafutia. Mwanaume yeote anahitaji sana kuheshimiwa, na anathamini kuonekana mwenye nguvu na mamlaka, aliyebolea au mtaalamu wa eneo/jambo flani, na makini katika kazi, lakini zaidi aliyefanikiwa.

Daima mwanaume anavutiwa au anahamasishwa na uwezo wake katika kuleta MATOKEO chanya. Haitoshi yeye hupenda zaidi kuongelea VITU na MADA zenye mashiko kuliko WATU na HISIA.

Mwanaume hupata motisha zaidi akionekana KUHITAJIKA, na anapoboreka au kusongwa na mambo hupenda kujitenga binafsi (peke yake), na

kuanza kufikiri kuhusu hilo jambo. Mwanaume kwa asili hawezi kufanya jambo zaidi ya moja kwa wakati mmoja, Na chochote anachozungumza au anachofanya mwanaume ni matokeo ya kile anachofikiri. Mwanaume daima huendeshwa na uhalisia(Facts) kuliko hisia(Feelings). Ni ngumu sana mwanaume kuonesha hisia zake, lakini pia ni ngumu sana mwanaume kukubali makosa na hata kufikia kuomba msamaha.

Ningeweza kuandika mamia ya Ufahamu wangu juu ya **WANAUME**, lakini kwa leo naishia hapa. Ninachojaribu kukuonyesha ni nguvu ya Ufahamu katika kukusaidia kujitambua na hatimaye kuishi kwa hekima. Ngoja nikuonyeshe tena Mwanaume hupenda/ huvutiwa zaidi kwa kuona kwa macho, lakini pia hisia ya Mwanaume juu ya tendo la ndoa ni kali isiyoelezeka, uhitaji wake ni kama chakula kwa kiumbe hai. Ahahahahahahahah.

3. Ni MCHAKATO!

“Mimi naenda njia ya ulimwengu wote; basi wewe uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume; uyashike maarifa ya BWANA, Mungu wako, uende katika njia zake, uzishike sheria zake, na amri zake, na hukumu zake, na shuhuda zake, sawasawa na ilivyoandikwa katika torati ya Musa, upate kufanikiwa katika kila ufanyalo, na kila utazamako;” 1 Wafalme 2:2,3

Mfalme Daudi anamuusia mwanae wa kiume Sulemani akimtaka awe hodari na ajionyeshe kuwa Mwanamume. Kwenye mstari wa tatu(3) anamfafanulia kwa undani yanayompasa kufanya, na mwishoni anamwambia upate kufanikiwa katika kila ufanyalo, na kila utazamako. Kumbe unaweza kuzaliwa wa kiume na bado ukashindwa KUJIONYESHA/KUDHIHIRISHA Uanaume. Kuna mchakato fulani lazima uupitie na ufaulu ili kuitwa MWANAUME halisi.

Leo tuna watu wazima wa kiume wengi ambao ndani yao bado ni WAVULANA. Ukijaribu kutafuta

Uanaume kwa sifa na tabia zao wala hauonekani. Wengi wao walikimbia au walikosa mchakato wa maandalizi wa kuwafanya wanaume. Kuna MWANAUME ndani ya kila Mvulana. Ndani ya kila Mvulana kuna MWANAUME, MUME na BABA. Na ili kumdhahirisha huyu MWANAUME, ni lazima huyu mvulana apitie mchakato wa maandalizi ya kiume ya kuwa MWANAUME.

KUBALEHE na kuweza kumpa mwanamke ujauzito sio ishara toshelevu ya kwamba wewe ni mwanaume. Kwenda jando na kupitia mafunzo ya kimila haitoshi wewe kuitwa MWANAUME. Ni muhimu sana familia, kanisa, jamii na taifa lifahamu kwamba lina wajibu wa kuwaandaa wavulana katika njia sahihi. Ni vizuri mvulana apate mafunzo sahihi ya kiimani, kifikra, kijamii ,kizalendo na hata kiufahamu yatakayomsaidia kujitambua na kuanza kuchukua hatua stahiki za kuwa Mwanaume. Ni lazima wavulana wapate mifano sahihi kwa kuona miongoni mwa jamii zinazowazunguka kwamba WANAUME HALISI ni watu wa namna gani. Waone kwa macho yao namna MWANAUME anavyobeba majukumu ya Uongozi, Mume na Baba.

Na hii haitoshi ni muhimu sana wavulana wapate walezi, wasimamizi(mentors) wa kuwaongoza katika njia na kanuni sahihi za kufanyika WANAUME. Wavulana wapate nafasi ya kujua misingi ya kimaadili, elimu ya mahusiano, bidii katika kazi na majukumu kwa ujumla, ili kuwawezesha kuwa WANAUME.

Ndugu yangu eeeh, umezaliwa wa kiume lakini unatakiwa kuwa MWANAUME. Kuwa Mwanaume ni Mchakato, ni lazima uandaliwe, maana UANAUME ni majukumu. Leo dunia imekosa kabisa WANAUME licha ya kuwa na mamilioni ya watu wanaozaliwa wa kiume kila leo. Jamii imekosa viongozi, Wanawake wamekosa Waume, na mamilioni ya watoto wamekosa BABA.

4. Ni MAJUKUMU!

“Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake,.....” Mwanzo 1:26,27

“Kesheni, simameni katika Imani, Fanyeni kiume, mkawe hodari” 1 Wakorintho 16:13

UANAUME ni majukumu, huwezi kuwa mwanaume halisi mpaka umetimiza wajibu wako kama mwanaume. Na mimi nimeona ni vema nikuletee hapa baadhi ya majukumu ya msingi ya mwanaume, kwenye ngazi zote kuanzia kwenye Familia, Kanisa, Jamii na Taifa kwa ujumla.

Mwanaume yejote aliyeumbwa na Mungu hupaswa kuwa na nafasi na majukumu yafuatayo;

1. **Ni KIONGOZI;** huwa mtu wa mbele (mbeba maono), mtu mwenye ushawishi na anayejua hatima njema. Ni mtu anayeijua njia, anayeonyesha njia na anayeifata hiyo njia ili

kuwapeleka wafuasi wake(Familia, Jamii, Kanisa na Taifa) kwenye hatima njema.

- 2.***Ni KUHANI;*** Mtu anayewaongoza watu katika KWELI ya Mungu, Anayewakutanisha watu na Mungu. Ni mtu wa Ibada, mtu wa Maombi, aliyejaa Neno la Mungu na kuwafundisha wengine. Mcha Mungu na mtu wa Maadili, anayejiепusha na maovu.
- 3.***Ni MPAJI;*** Mtu anayehudumia familia na jamii kwa mahitaji mbalimbali.Yeye ndiye msingi na nguzo ya mahitaji ya Familia. Hujali na kuwatunza watu wake.
- 4.***Ni MLINZI;*** Mtu anayelinda familia na watu wake Kiroho, Kihisia, Kimaadili na Kimwili. Huhakikisha Usalama wa watu wake na eneo lake wakati wote.
- 5.***Ni MWEZESHAJI;*** Huwa mtu anayewezesha wengine kwenye mambo mbalimbali, kupitia yeye watu hupata namna ya kupiga hatua kwenye Nyanja mbalimbali.
- 6.***Ni MWALIMU;*** Huwa Mtu anayefundisha watu wake mambo mbalimbali kuanzia mambo ya kiroho, kimaadili, kazi na mambo mengine mengi muhimu.

7. *Ni MSHAURI;* hushauri watu wake juu ya kutatua, kupenya au kufanya mambo mbalimbali kwa ubora na ufanisi. Mara zote huwa na maarifa ya kutosha kushauri mambo kwa uchanya na usahihi.

8. *Ni MKUZAJI na MWENDELEZAJI;* huona jambo jema kwa watu wake kama Uwezo, Vipaji, Huduma, Karama, Ubunifu, Ugunduzi n.k, Na humwendeleza mtu ili awe bora kwenye eneo husika.

Huyu ndiye MWANAUME ambaye familia, kanisa, jamii na taifa linamtarajia kutoka kwako **Mvulana**. Na nikukumbushe tu tena kwamba Uanaume ni Uwajibikaji sio jinsia.

5. Ni USHIRIKA na MUNGU!

“...., Nimemwona Daudi, mwana wa Yesu, mtu anayeupendeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote” Matendo 13:22

“Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu” Zaburi 42:1

“Neno Moja nimelitaka kwa BWANA, Nalo ndilo nitakalolitafuta, Nikae nyumbani mwa BWANA Siku zote za maisha yangu, Niutazame uzuri wa BWANA, Na kutafakari hekaluni mwake” Zaburi 27:4

Hakuna ukamilifu wa MWANAUME bila Mungu. Kama kuna kitu kila mwanaume anakihitaji kuliko kitu kingine chochote ni UHUSIANO na USHIRIKA wa karibu sana na Mungu. Mwanaume wa kwanza Adamu alipoumbwa alipuliziwa pumzi na Mungu, na kwayo akawa mtu hai. Mwanaume anamhitaji Mungu Maishani mwake kuliko anavyohitaji pumzi.

Daudi anasma kama Ayala aioneavyo shauku mito ya maji ndivyo nafsi yake inavyomuonea shauku Mungu, na tena anasema neno moja amelitaka na hilo ndilo analolitafuta nalo ni kukaa nyumbani (uweponi) mwa BWANA siku zote za Maisha yake. Halafu tunaona Mungu mwenyewe anasema kwamba Daudi ndiye mtu anayeupendeza moyo wake, kwa kuwa anayafanya Mapenzi yake yote. Hii inamaanisha kwamba Mwanaume mwenye shauku, kiu, ari na dhamira ya kumwabudu Mungu kwa Roho na Kweli, yaani Mwanaume wa Ibada, ndiye anayeupendeza moyo wa Mungu, na kupitia huyo utukufu wa Mungu huonekana.

Moja ya kigezo muhimu cha kufanyika MWANAUME halisi, ni kuwa mwanaume wa Ibada mwenye Ushirika wa Karibu na Mungu. Na mimi leo nataka nikukumbushe kidogo tu mambo ya kuzingatia kuelekea kuwa Mwanaume wa Ibada kama Daudi.

1. Mwanaume aliyejaa ***NENO LA MUNGU***, anasoma, anatafakari na analiishi Neno.
2. Mwanaume wa ***MAOMBI***, anayeomba binafsi, anayefunga na kusikiliza kutoka kwa BWANA

3. Mwanaume aliyejawa na ***ROHO MTAKATIFU***, Kila wakati anamsikiliza na kumtii Roho Mtakatifu.
4. Mwanaume wa ***IMANI***, anayeishi kwa uhakika pasipokuona akimwamini BWANA.
5. Mwanaume ***MTOAJI***, mtu anayemweshimu na kumpenda Mungu kwa Mali zake.
6. Mwanaume wa ***SIFA***, anayemsifu BWANA kila inapoitwa leo kwa uzuri wake.
7. Mwanaume ***MTUMISHI***, anayetumia vipaji, karama, huduma, mali, elimu, kazi, familia na kila kitu chake kumtumikia BWANA.

Mwaaume yejote akamiliki mpaka amejenga ushirika wa karibu na Mungu. Mahusiano ya Karibu na Mungu huleta tija katika MAJUKUMU ya mwanaume.

6. Ni UTOFAUTI na MWANAMKE!

“Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba” **Mwanzo 1:27**

“na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu” **Mwanzo 2:22**

Ukishazaliwa wa kiume maana yake wewe sio wa kike, unapoitwa mvulana maana yake wewe sio msichana, halikadhalika unatarajiwa uwe mwanaume na sio mwanamke. Kama ndivyo tunaamini utakuwa mume na sio mke, na utakuwa baba wala sio mama. Ikiwa yote niliyosema ni sawa, basi tambua unatakiwa kudhihirisha wewe ni mwanaume.

Nisikilize sasa, Kuna tofauti nyingi sana kati ya wanaume na wanawake, kuanzia kwenye muonekano mpaka kwenye majukumu. Ni hatari na aibu sana mwanaume kuwa kama mwanamke kwa namna yoyote ile. Wanaume na wanawake wana tofauti kubwa sana kuanzia KIBAOLOJIA, KIHISIA, KIFIKRA, KISAIKOLOJIA na hata KIROHO. Nikitaka kuandika tofauti zote nahitaji kitabu kizima

kingine. Hapa naweza kupata mifano michache walau, lakini kwanza labda nikuulize utajisikiaje mtu akikwambia ***WEWE NI MWANAMKE TU au WEWE MBONA MAMA tu!***, Bila shaka utajisikia vibaya sana, Unajua kwanini?, ***Sio kwa sababu kuwa mwanamke au mama ni vibaya la hasha, ila sio asili yako.***

Leo hii tuna balaa limeingia kwenye jamii yetu, huwezi kuamini kwamba leo tunao vijana na watu wazima wa kiume, ambao wameamua kuwa wanawake kabisa. Yaani tabia na mienendo yao ni kama wanawake, na haitoshi kuna wengine wameamua mpaka mionekano yao imekuwa ya kike. Yaani badala ya kutoa mahitaji wao wanapokea tu, badala ya kuwa viongozi wao wanaongozwa, badala ya kuoa wanaolewa, badala ya kujishughulisha wao wanakaa tu kwa raha zao, Nakuombea isiwe kwako katika jina la Yesu.

Let a man be a man (*Acha Mwanaume awe mwanaume*) na let a woman be a woman (*Acha mwanamke awe mwanamke*). Familia zetu za leo ni aibu tupu, na hata baadhi ya makanisa ni aibu tupu. Kina mama wamekuwa vichwa na wahangaikaji wa familia, kina baba hawaonekani makanisani, Watoto

wanaranda randa mitaani wamekosa muongozo wa kina Baba, Baba zao hawaonekani na waliopo hawajitambui, **WAKO WAPI WANAUUME LEO?**.

Tangu Edeni, wakati wa anguko na hata baada ya anguko, kuja kwa Yesu na mpaka leo tunapoishi chini ya Agano la Neema, tofauti za muonekano, majukumu na wajibu kati ya Mwanamke na Mwanaume zipo wazi sana sana.

Nisikilize tafadhali, maadam umezaliwa wa kiume, kuwa mwanaume, simama kwenye nafasi yako ipasavyo. Ukumbuke Mungu alikusudia wewe uwe **MWANAUME** na wala sio **MWANAMKE**, angetaka uwe mwanamke mbona ungalizaliwa tu wa kike tena kirahisi, ahahahahah.....!

7. Ni UTUKUFU WA MUNGU!

“Kwa maana haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume” 1 Wakorintho 11:7

Unajua bhana sisi tumeumbwa kwa sura na kwa mfano wa Mungu. Na alichokuwa amekusudia Mungu tangu Adamu, ni sisi kuudhihirisha ule Uungu kwa namna ambayo itampa utukufu. Yaani ni hivi, Mwanaume aliumbwa ili kuleta ile picha halisi ya Mungu duniani, na ndio maana hilo andiko hapo juu linasema MWANAUME ni mfano na utukufu wa Mungu.

Mwanaume anatakiwa au anapaswa kudhihirisha zile sifa na tabia za Mungu hapa duniani, kiasi kwamba kupitia hizo Mungu ajitwalie Utukufu. Adamu wa kwanza pale bustanini alishindwa kusimama kwenye hiyo nafasi, lakini uzuri kupitia Adamu wa pili ambaye ni Yesu Kristo tulirejeshewa ile nafasi na ule Uungu tena.

Mtu wa kiume anaposimama kwenye nafasi yake kama MWANAUME, MUME, na BABA anakuwa mfano halisi wa Mungu na hii inampa Mungu

utukufu. Ikumbukwe tu kwamba Yesu alikuwa MWANAUME, na alifanyika MUME kwa Kanisa ambalo ni Bibi Harusi na ndio mwili wake. Na Yesu Kristo yaani Mwana, Mungu halisi katika utatu wa Mungu. Ni Dhahiri Mungu kwetu ni BABA, tena BABA wa milele, amekuwa Baba ambaye amesimama daima katika nafasi yake kwa ufanisi mkubwa usioelezeka.

Na hii ndio maana mtu wa kiume anaposimama kwenye nafasi yake vizuri kama MWANAUME, MUME na BABA, akitimiza wajibu wake na majukumu yake kama inavyostaili, anaakisi ile tabia na sifa halisi za Mungu kama BABA, MUME (Yesu). Hivyo anafanyika kuwa mfano na utukufu wa Mungu.

Ukitaka kuwa MWANAUME ambaye ni mfano na utukufu wa Mungu kusudia kusimama kwenye nafasi yako. Kamwe usizembee katika kujenga na kuimarisha uhusiano/ushirika wako na Roho mtakatifu. Roho Mtakatifu atakuwezesha kusimama kwenye nafasi yako huku akikusaidia (*Ni Msaidizi*), akikuombea(*Ni Mwombezi*), akikufariji (*Ni Mfariji*), akikushauri(*Ni Mshauri*), akikufundisha (*Ni Mwalimu*) na mengine mengi.

Lakini pia utapokea na kuishi TUNDA LA ROHO, utakuwa ni MWANAUME mwenye ***UPENDO, FURAHA, AMANI, UVUMILIVU, UTU WEMA, FADHILI, UAMINIFU, UPOLE na KIASI***, katika yote haya utafanyika MWANAUME wa Mfano na Utukufu wa Mungu.

8. Ni Nguvu ya MABADILIKO!

**“Nami nikatafuta mtu mionganini mwao,
atakayelitengeneza boma, na kusimama mbele
zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi.....”**
Ezekiel 22:30

**“...; lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu
aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka,
atetemekaye asikiapo neno langu” Isaya 66:2**

**“Na watu watapajenga mahali palipokuwa ukiwa;
utaiinua misingi ya vizazi vingi nawe utaitwa,
Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na
Mwenye kurejeza njia za kukalia” Isaya 58:12**

Mwanaume mmoja akisimama kwenye kusudi na nafasi yake sawasawa na alivyokusudia Mungu huokoa familia, kanisa, jamii na hata taifa. Lakini pia mwanaume mmoja akikengeuka na kuamua kufanya yasiyofaa anaweza kuleta balaa na janga kwenye familia, jamii, kanisa na hata taifa.

Wakati wote Mungu amekuwa akitafuta na kuinua mtu mmoja tu kwa ajili ya kusimamia kusudi ambalo hufanyika upenyo na amani ya wengi. Hebu angalia, kupitia Ibrahimu sisi sote tumebarikiwa, kupitia

Yusufu Misri yote walipona na janga la njaa, kupitia Musa wana wa Israeli walitoka utumwani Misri, kupitia Nehemia ukuta wa Yerusalem ukajengwa upya, kupitia Gideoni Israeli wakashinda vita, na kupitia Yesu sisi sote tumekombolewa. Na hata sasa kupitia mtu mmoja aliyesimama kwa uaminifu mbele za Mungu mambo yanatokea.

Nataka nikuhakikishie ukisimama vizuri kiume kama inavyotakiwa yako mambo Mungu atafanya kwenye familia yako, ukoo wako, shulenii kwako, chuoni kwako, kanisani kwako, kwenye jamii yako na hata kwenye taifa lako kupitia wewe.

Shime Wanaume, hebu kila mmoja wetu asimame sasa kiume kwenye nafasi yake ili, Mungu afanye mabadiliko kupitia sisi. Ipo Huduma ndani yako, Lipo Shirika ndani yako, Lipo wazo ndani yako, Ipo taasisi ndani yako, Upo msukumo na shauku ndani yako, ambayo ukisimama vizuri kwenye nafasi yako kama mwanaume, Mungu atakutunia kuleta MABADILIKO chanya kupitia hivyo.

Simama Kiume, Jionyeshe mwanaume, Kaa kwenye nafasi yako, Simama kwenye zamu yako inavyotakiwa, Tambua wakati na majira ya kujiliwa,

halafu utamuona Mungu akikutumia WEWE na wala sio nyie katika kuleta MABADILIKO mahali fulani kwa UTUKUFU WAKE. **Mimi nasimama KIUME, Wewe je?.**

9. Ni UTHUBUTU.

“Kesheni, simameni imara katika Imani, fanyeni kiume, mkawe hodari” 1 Wakorintho 16:13

“Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi” 2 Timotheo 1:7

“Tupa chakula chako usoni pa maji; Maana utakiona baada ya siku nyingi. Mwenye kuuangalia upepo hatapanda; naye ayatazamaye mawingu hatavuna ” Mhubiri 11:1,4

UTHUBUTU ni hali ya kufanya jambo jipya kwa ujasiri bila kuogopa hatari wala hasara. Kila mwanaume ndani yake ameumbiwa uthubutu, na kwa sisi tunaomwamini Mungu, tunaoenenda kwa Imani wala sio kwa kuona ni rahisi zaidi kuthubutu. Watu wengi wamepoteza fursa na nafasi nyingi kwa kushindwa KUTHUBUTU.

UTHUBUTU, ni kuchukua hatua ya Imani kufanya jambo huku ukimwamini BWANA kwamba atatenda kupitia hilo. Kwenye uthubutu huwa hakuna neno Hasara, bali kuna kufanikiwa au kujifunza jambo jipya au njia mpya ambayo ni bora zaidi.

Mara nyingi Uthubutu huwa hauangalii hali ya nje au mazingira ama watu wanasemaje, ILA amani ya ndani ambayo ndio ishara ya mtu kusonga mbele kwa Roho Mtakatifu.

Kama Daudi angesikiliza maneno ya watu NA angeliangalia ukubwa wa Goliath asingelithubutu kwenda na kupigana nae. Kama Nehemia angeliangalia ukubwa wa ukuta na mazingira halisi, asingelithubutu kwenda nchini kwao na kujenga tena. Na kama Kalebu angeliangalia ukubwa wa yale majitu, asingemshauri Yoshua kwenda kupigana na kuitamalaki nchi. Kwenye uthubutu unapoamua kuacha kutazama mazingira, na badala yake kumtazama Mungu, kufanikiwa ni lazima. Lakini ukikomaa kuyatazama mazingira na hali, pamoja na kusikiliza maneno ya watu, kutothubutu kuko nje nje yaani.

Mwanaume daima ni mtu wa kudhubutu, asili ya mwanaume ni kutoogopa hatari na hasara. Na ndio maana mwanaume ni mtu wa vita, kila wakati hupambana na mambo mbalimbali. Mwanaume muoga ni hatari kwa familia, jamii na hata Taifa. Mwanaume halisi hupiga hatua mpya kila siku,

hutoka nje ya bosi, huenda maili zaidi (extra mile), huondoka kwenye eneo salama (comfort zone). Huchukua hatua ya Imani katika kufanya mambo mapya, kujaribu fursa mpya, kwenda eneo jipya, ili tu kupata namna ambayo wanaomtegemea wataishi Maisha mazuri na salama.

Narudia tena Mwanaume ni mtu wa uthubutu, Ibrahimu alitoka kwenye nchi yake na kwenda asipopajua (alithubutu), alichukua hatua ya Imani. Ni muhimu sana tuwe watu wa uthubutu huku tukimwamini Mungu aliye upande wetu kila siku.

10. Ni UTIMILIFU wa NDOTO zako!

“Pasipo maono, watu huacha kujizuia, Bali ana heri mtu aishikaye sheria ” Mithali 29:18

Mwanaume kama KIONGOZI ni muhimu kuwa na ndoto na maono, ambayo kwayo atalitimiza KUSUDI la Mungu, pamoja na kuwawezesha wafiasi wake kuelekea Hatma njema.

Kama kwa Yusufu, utimilifu wa ndoto au maono sio jambo jepesi. Ni muhimu mwanaume ajue anatakiwa kupambana kwa kila hali huku akimtegemea Mungu, ili aliishi kusudi la Mungu lililotafsiriwa katika ndoto au maono kwa usahihi.

Ndoto yoyote ili iwezee kutimia ni lazima iwekwe katika mfumo au mchakato rahisi wa utekelezaji. Ndoto Kubwa kabisa huweza kugawanywa katika matukio na nyakati ambazo zitarahisisha utimilifu wake. Kwa mfano ndoto inaweza kugawanywa katika malengo (Goals) mbalimbali ambayo yatawekewa muda maalumu wa utekelezaji. Halafu hayo malengo yanaweza kugawanywa pia katika mipango (Plans) mbalimbali, na kwa kila mpango, ukawekwa mkakati(strategy) ili kukamilisha. Na hatimae kukawa na shughuli (activities) za kufanya kwa kila mkakati. Hii kwa ujumla wake huleta utimilifu wa

ndoto au maono. Zipo hatua mbalimbali ambazo mwanaume lazima azipitie kuelekea utimilifu wa ndoto zake.

Yusufu alipoona ile ndoto alidhania ingekuwa rahisi tu kutimia. Hakujua kuna vipindi na matukio ambayo ilibidi kuyapitia mpaka utimilifu wa ndoto yake. Kama asingelikomaa kiume huku akimtegemea Mungu, kwa hakika angebaki kuiona ndoto yake kama picha ya mbali na kamwe asingeifikia.

Hebu angalia kutoka kunusurika kuuwawa, kutumbukizwa kisimani, kuuzwa kwa mfanyabiashara, kunusurika kubakwa, kupelekwa gerezani, na mwishoni sasa anafika kwenye kile alichokiona. Kwa akili ya kawaida tusingekubali mtu aliyeptia mambo haya anaweza kuja kuwa Waziri Mkuu tena kwenye nchi kubwa kama ile, halafu ya Ugenini.

Ni vizuri Mwanaume ufahamu kwamba mawazo ya Mungu sio kama mawazo yetu NA njia zake sio kama njia zetu. Nikutie moyo mwanaume, ndoto na maono uliyonayo ikiwa yanaakisi kusudi la Mungu maishani mwakoni lazima yatafanikiwa kufikia utimilifu wake. Haijalishi hali na mazingira yanaonekanaje, endelea

kufanya sehemu yako huku ukimtegemea Mungu kwa Imani. Daima Ahadi za Mungu ni KWELI NA AMINA. Endelea kuomba huku ukimsikiliza Yeye, naye atayanyosha mapito yako kuelekea utimilifu wa Ndoto yako sawasawa na kusudi lake. Na iwe kwako katika jina la Yesu.

11. Ni UGUNDUZI na UCHOCHEZI WA HAZINA!

**“Kipawa ni kama kito cha thamani machoni pake
yeye aliye nacho; kila kigeukiapo hufanikiwa”
Mithali 17:8**

**“Usiache kutumia karama ile iliyomo ndani yako,
uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya
wazee” 1 Timotheo 4:14**

**“Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee
karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa
mikono yangu.” 2 Timotheo 1:6**

Mungu alipokuumba wa kiume, aliwekeza ndani yako hazina mbalimbali ambazo ni viwezesho kwa wewe kuliishi kusudi lake kwa ukamilifu. Hazina hizi ni vipawa, vipaji, uwezo, akili ubunifu, na huduma mbalimbali. Hivi vyote tayari vipo ndani yako, lakini usipogundua hautavitumia, Daima hazina hizi huakisi au huendana na kazi au wajibu au kusudi Mungu alilokuitia kufanya hapa duniani.

Ni muhimu tugundue kwamba hazina hizi zinatusaidia kutimiza kusudi la Mungu,

zinatufanikisha kwenye maisha yetu ya kila siku NA zinaweza pia kutuweka pamoja na wakuu.

Lakini tusipogundua kwamba tunazo, na tukajua ni zipi, na kisha tukaanza kuzichochea zitumike, hazina hizi zitakuwa ni bure.

Paulo alimwambia kijana wake Timotheo zaidi ya mara moja, akimsisitiza kutumia karama zilizopo ndani yake. Mara ya kwanza anamwambia USIACHE kuitumia, na mara ya pili anamkumbusha tena anamtaka AICHOCHEE karama ya Mungu iliyo ndani yake.

Mambo matano ya msingi ili kugundua na kuchochea hazina zilizo ndani yako:-

1. OMBA:- Mwombe Mungu Baba kwa Roho wake Mtakatifu akusaidie ugundue kila hazina aliyowekeza ndani yako sawasawa na kusudi lake.

2. GUNDUA:- Baada ya kuomba Mungu atakupa kugundua kila Hazina aliyowekeza ndani yako hatua kwa hatua. Utaanza kupata wepesi na urahisi wa kufanya mambo kwa kipawa, kipaji, huduma na karama iliyopo ndani yako.

3. IKUBALI:- Ukishagundua HAZINA zilizopo ndani yako, Zikubali na zipende, na Kaa sawa ili uweze kuzitumia kwa Utukufu wa MUNGU.

4. NOA:- Unanoa kipawa, karama, kipaji na huduma kwa kujifunza namna sahihi ya kuzitumia kwa ufanisi na ubora. Jifunze kwa waliokutangulia na wanaojua kukuzidi, ikiwezekana nenda mafunzo maalum, kaa chini ya walezi au washauri, Tumia kila njia inayowezekana kujifunza zaidi ili kunoa hazina zako.

5. TUMIA:- Hii ndo hatua ya muhimu baada ya kugundua, kuweka sawa na kuzinoa hazina zilizopo ndani yako. Ni kuzitumia sasa kwa bidii ili kukamilisha Kusudi la Mungu.

Mwanaume halisi hugundua na kuchochea hazina zilizopo ndani yake ili kutimiza kusudi la Mungu maishani mwake.

12. Ni mbali na UVIVU na UZEMBE!

“Mkono wa mwenye bidii utatawala; Bali mvivu atalipishwa kodi,” Mithali 12:24

“Usipende usingizi usije ukawa maskini, Fumbua macho yako nawe utashiba chakula” Mithali 20:13

“Akasema, itwae mishale; akaitwaa. Akamwambia mfalme wa Israeli, piga chini; akapiga chini mara tatu, akaacha. Yule mtu wa Mungu akamkasirikia, akasema, ingalikupasa kupiga mara tano au sita; ndipo ungaliipiga Shamu hata kuiangamiza; bali sasa utaipiga Shamu mara tatu tu” 2 Wafalme 13:18;19

Pale Edeni Mungu alipomuumba Adamu, alimpa kwanza KAZI kabla ya MKE. Asili ya Mwanaume ni kazi au majukunu. Na ndio maana mwanaume hapaswi kuwa mvivu au mzembe hata kidogo.

Ni aibu sana ukawa wa kiume halafu eti haupendi kabisa kufanya kazi au hautaki kufanya kazi sana.

Unagusa tu kazi kidogo alafu unalalamika umechoka au unasema bila aibu kwamba umechoka. Vijana eeh, ukitazama tu majukumu ya mwanaume ndani ya familia ambayo ni Mpaji, Mlinzi, Mwezeshaji, Kuhani, Mtunzaji na nyinginezo, utagundua kwamba

ili uyatimize kwa kiwango unachotakiwa LAZIMA UFANYE KAZI.

Ili sifa na nafasi yako kama mwanaume,Mume na Baba zibaki zikiheshimiwa na kukubalika, ni lazima ufanye kazi. Wala hakuna msichana ambaye yuko tayari kuolewa na mvulana asiye na kazi ya kufanya, au asiyetaka kufanya kazi. Ni lazima kama mwanaume ujiture na ufanye bidii ya kuwa mtafutaji na mpambanaji ili kusimama vema katika nafasi yako.

Leo tuna wimbi la vijana wengi wanaofanana kitabia na yule mfalme wa wakati wa Elisha mtu wa Mungu, ambaye kwenye ile 2 Wafalme 13: 18,19 unaona Elisha anamuagiza apige chini. Mfalme alipiga chini mara tatu tu halafu akaacha. Elisha anakasirika anamwambia ultakiwa kupiga mara tano au sita, Na tena anamwambia angepiga mara tano au sita angawaangamiza kabisa maadui zake.

Vijana wa kiume hivi leo hawataki kujituma zaidi, wanagusa gusa kazi kidogo wanaacha. Hawajui kwa kadri unavyofanya zaidi, ndivyo ambavyo wepesi kwenye maisha yako na kudhihirisha UANAUME wako. Saa ndio hii, na Wakati ndio huu, Shime

Wanaume twendeni tukafanye kazi na BWANA
atazibariki kabisa kabisa kazi za mikono yetu.

13. Ni UWAKILI Mwema!

“Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadri ya uwezo wake; akasafiri” Mathayo 25:15

“Yule bwana akamsifu wakili dhalimu kwa vile alivyotenda kwa busara; kwa kuwa wana wa ulimwengu huu katika kizazi chao wenyewe huwa na busara kuliko wana wa nuru” Luka 16:8

Tangu Edeni mwanaume alipewa na Mungu dhamana ya kumiliki, kutunza, kutawala, na kusimamia kila alichouumba Mungu. Huu ndio unaitwa UWAKILI, Sote tunajua ya kwamba NCHI NA VYOTE VIIJAZAVYO ni mali ya BWANA, dunia na wote wakaao ndani yake.

Kama MWANAUME, wewe ni WAKILI, unapaswa kumiliki, kulinda, kuendeleza, kutunza, kutawala, na kusimamia kila ambacho Mungu amekupa dhamana kwayo. Ukumbuke hata Maisha yako si yako, uliletwa kwa KUSUDI la Mungu, haupaswi kuishi kama unavyotaka wewe bali kama atakavyo Mungu.

Kama wale watumwa wawili walivyokuwa waaminifu kwa talanta alizowapa BWANA wao, yule wa Tano akazalisha tano Zaidi, na yule wa mbili

akazalisha mbili Zaidi. Ni muhimu na wewe kuwa mwaminifu kwa kila ambacho mungu amekupa dhamana. Ni hekima kuwajibika kama **WAKILI** kwenye **MUDA**, **FEDHA**, **UWEZO**(vipawa,vipaji,huduma,karama), **WATU**, **TAARIFA**, **RASILIMALI** mbalimbali na kila ambacho Mungu amekupa kumiliki na kutawala.

Kanuni nne muhimu za UWAKILI zitakazokusaidia kila wakati kutambua unachopaswa kufanya kama **WAKILI**. Karibu tujifunze pamoja:-

- i. Kanuni ya UMILIKI;** unapokuwa **WAKILI** unafanyika mmiliki halali wa rasilimali za **BWANA** wako aliyekupa dhamana kwa kukuamini.
- ii. Kanuni ya UWAJIBIKAJI;** unapokuwa **WAKILI** unakuwa muwajibikaji mkuu wa rasilimali za **BWANA** wako. Lolote likitokea wewe ndio mhusika mkuu wa kuelezea kinagaubaga. Mwisho wa siku utatoa mrejesho mbele ya **BWANA** wako.
- iii. Kanuni ya MAJUKUMU;** unapokuwa **WAKILI** majukumu (utendaji kazi wote) wa rasilimali za

Bwana wako unakuwa juu yako. Na ndio maana unatakiwa kuendeleza na kuzalisha faida.

iv. Kanuni ya ZAWADI; unapokuwa WAKILI mwisho wa siku baada ya kupeleka mrejesho ya kazi aliyokuachia BWANA wako unapewa Ujira/ pongezi kutegemeana na namna ulivyofanya.

Mungu ambaye ni BWANA wetu amemkirimia kila mmoja wetu na vingi. Ni muhimu usimame kiume na utekeleze kazi yako kama WAKILI ili mwisho wa siku upate ujira mwema. Natamani sote tuambiwe hongera mtumwa mwema na mwaminifu, tusiwe kama yule wa Talanta moja aliyeichimbia chini.

14. Ni mbali na UASHERATI!

“Ikimbieni zinaa, kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwiili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe. Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu?.....” 1 Wakorintho 6:18,19

“Nilifanya Agano na macho yangu; Basi nawezaje kumwangalia msichana?” Ayubu 31:1

“Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti” Yakobo 1:15

Moja ya maeneo yanayotesa wanaume ni zinaa, yaani Uasherati(Kwa ambao hawajaoa) na Uzinzi(kwa ambao wameoa). Unajua asili ya mwanaume ni kuvutiwa na tendo la Ndoa(SEX), na kwa sababu wanaume huvutiwa kwa kuona wanawake, hili limekuwa tatizo kubwa. Ayubu alisema alipatana na Macho yake kwamba hawezi KUMWANGALIA, na sio KUMWONA msichana. Unajua ukitaka USIONE msichana njia ni moja tu HAMA duniani, ila KUANGALIA ni maamuzi yako. KUANGALIA ni kumwona msichana na kuanza kumtafakari kwa hisia

za kingono kiasi cha kuamsha tamaa za ngono, na hata kuchukua hatua ya kumtongoza na hatimaye kulala nae. Ndio Biblia inasema tamaa ikichukua mimba huzaa dhambi.

Daudi yeye alikosa kazi akawa anapunga upopo ghorofani, akamwona mwanamke anaoga akaamua kumwangalia, mwisho wa yote aliishia kufanya dhambi. Maana tamaa yake ilichukua mimba ikazaa dhambi, na dhambi yake ikazaa mauti (Kupoteza mahusiano na Mungu). Ukikosa kazi ya kufanya mwanaume, shetani atakupa kazi ya kufanya. Daudi aliacha kwenda vitani shetani akampa la kufanya. Yusufu yeye alitengwa mara kadhaa akachomoa, na siku alipobanwa pabaya **AKAKIMBIA**. Kwa mwanaume zinaa ni hatari sana, epuka mazingira yote yanayoweza kupelekea wewe kukamatwa na hii dhambi.

Madhara anayopata mwanaume kwenye zinaa ni makubwa zaidi kuliko anayopata mwanamke. Ukitolewa Mithali 6 utaona anavyoainisha, tena anasema usiwape wanawake nguvu zako. Thamani, Heshima, Uhuru, Ujasiri, Nguvu na mamlaka yako hupotea pale tu unapolala na mwanamke, na ndio

maana ukishalala na mwanamke ambaye sio mke wako kamwe hawezi kukuheshimu tena hata kama awe nani.

Kwa wakati sahihi ndani ya ndoa , Tendo la ndoa ni Ibada, Nje ya wakati, kabla ya ndoa Tendo la Ngono ni dhambi. Nafsi yako huunganishwa na mtu asiye sahihi (soul tie) na balaa, nuksi, mikosi kutoka kwake huambatana nawe pia. Ya nini kupoteza utukufu wa Mungu ndani yako kisa kitendo cha dakika tano, ili hali wakati wako sahihi unakuja.

Epuka vishawishi na mazingira Ngono yote, sikiliza, soma na angalia vitu sahihi. Epuka kukaa faragha na msichana, epuka kuchat yasiyofaa na msichana, Epuka kuanzisha mahusiano na msichana yejote yasiyo na muelekeo wa Ndoa Mtakatifu.

Hebu jaza Neno la Mungu ndani yako, Ishi Maisha ya Maombi, Jenga uhusiano Imara na Roho Mtakatifu. Mwili wako ni Hekalu la Roho Mtakatifu, litunze na lithamini sana.

15. Ni kwa MSINGI na KIELELEZO!

“Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na Imani na usafi” 1 Timotheo 4:12

“Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli” 2 Timotheo 2:15

“Kama msingi ikiharibika, Mwenye haki atafanya nini?” Zaburi 11:3

Uimara na Uzuri wa jengo lolote unatokana na uimara wa msingi hilo jengo . Msingi ukiwa mbovu na dhaifu, hata kama jengo linaonekana zuri namna gani, ipo siku tu litaanguka na pengine mahali pale pasionekane tena. Msingi wa mwanaume ni Mungu, Na msingi wa familia, kanisa, jamii na taifa ni mwanaume. Mwanaume akishindwa kusimama kwenye nafasi yake vizuri kama msingi, Familia, Kanisa, Jamii na Taifa litaanguka. Ukiona mahali familia inasuasua jua kabisa Baba ameshindwa kusimama kwenye nafasi yake, Ukiona taifa halieleweki jua kabisa wanaume wa hilo Taifa ni dhaifu na wasiojitambua.

Na ili mwanaume akae vizuri kama msingi, ni lazima awe na mahusiano na ushirika mzuri na Mungu, ambaye ndiye msingi na chanzo cha mwanaume. Ukipoteza mahusiano na mawasiliano sahihi na msingi na chanzo chako, umepoteza ustadi wako. Hivyo ni vema mwanaume akae na adumu kwenye msingi wake, ili naye awe ni msingi imara wa familia, jamii, kanisa na Taifa kwa ujumla.

Mwanaume kama kiongozi yeye ni kielelezo au mfano katika mambo yote. Daima mwanaume anatakiwa kukaa mbele akiongoza familia na maeneo mengine juu ya kumcha Mungu, kupenda na kuheshimu wengine, kufanya kazi kwa bidii, kusimamia na kuishi maadili kwa uchanya, kuhudumia wengine, kuwawezesha wengine nakadhalika. Mwanaume lazima ajionyeshe kwamba anakubaliwa na Mungu, anajulikana na Mungu na tena anamjua Mungu. Kamwe mwanaume usiruhusu yejote kudharau nafasi yako, bali daima ilinde na kuitunza.

Nikakuta mahali fulani wameandika ***“A Father is the son’s first hero and daughter’s first love”***

Mwanaume lazima afanyike kielelezo kwa mwanae wa kiume kama Mwanaume, Mume na Baba bora. Lakini pia ni muhimu apande fikra na mitazamo sahihi kwa mabinti zake juu ya wanaume, waume na Baba. Mwanaume akishindwa kusimama kama msingi na kielelezo ni janga kwa familia, kanisa, jamii na taifa kwa ujumla.

16. Ni MISIMAMO na MIPAKA!

“Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia BWANA, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng’ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA” Yoshua 24:15

“..... Nifanyaje ubaya (uovu) huu mkubwa nikamkose Mungu? Akawa akizidi kusema na Yusufu siku baada ya siku, lakini hakumsikia alale naye, wala aongee nae” Mwanzo 39:9,10

“Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa; basi akamwomba yule mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi ” Danieli 1:8

Kuwa na misimamo thabiti isiyotetereshwa pamoja na kuweka wazi mipaka yako, ni moja kati ya sifa na tabia muhimu za mwanaume. Mwanaume halisi huwa anatambua na kuzisimamia TUNU zake bila kubabaishwa na yejote. Mwanaume halisi husimamia UKWELI hata kama mwisho wa siku

atabaki mwenyewe, maadam tu anachokisimamia ni sahihi kwa mujibu wa Imani na maadili yake.

Yoshua aliwaambia Wanawaisraeli wachague wanaemtumikia ila akasema wazi msimamo wake kwamba ye ye na nyumba yake watamtumikia BWANA. Danieli binafsi hata bila wenzake aliweka wazi mpaka wake wa kutojinajisi kwa chakula cha mfalme. Yusufu nae alisimamia msimamo wake mwanzo mwisho kiasi cha mwisho wa siku kuwekwa gerezani. Wako wapi wanaume leo wanaoweza kusimamia TUNU zao huku wakiweka wazi misimamo na mipaka yao?.

Wewe kama mwanaume ni lazima na muhimu familia, marafiki, ndugu na jamaa, kazini na maeneo mengine mbalimbali watu wafahamu misimamo na mipaka yako. Mwanaume asiyeweka wazi au asiyetambulika kwa misimamo na mipaka yake hubebwa na kila jambo. “If you don’t stand for something, anything will carry you”

Ni vema ufahamike wazi wewe ni mtu wa namna gani?. Misimamo na mipaka humsaidia mtu kufanya

maamuzi mbele ya watu kwa urahisi zaidi. Misimamo na mipaka humtambulisha mtu.

Mwanaume huwezi kufanya kila kitu, Hauwezi kwenda kila mahali, hauwezi kuambatana na kila mtu, hauwezi kuongea na kila mtu, na zaidi haufai kuwa Vuguvugu. Naandika tena ni lazima watu watambue misimamo na mipaka yako ili wajue wewe ni mtu wa aina gani. Misimamo na Mipaka inayotokana na Neno la Mungu humsaidia mwanaume kuliishi kwa ushindi kusudi la Mungu hapa duniani.

17. Ni UFANISI na UBORA!

“Na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza mfalme, akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake.” Danieli 1:20

Kufanya mambo kwa UFANISI na UBORA ni moja kati ya sifa muhimu za Mwanaume. Mwanaume anapoamua kufanya jambo huwa anaweka akili, na nguvu, na uwezo wake wote kwenye hilo jambo, na kuhakikisha kwamba linatoka katika UBORA unaohitajika na zaidi.

UFANISI ni kufanya jambo kwa usahihi kama linavyotakiwa kufanyika, UBORA ni kutumia nguvu, akili na uwezo wote kwa kiwango cha juu sana kufanya jambo. Dunia leo inatawaliwa na watu wanaofanya mambo kwa UFANISI na UBORA.

Na mimi nimeona niweke baadhi ya mambo ya kukusaidia mwanaume kufanya mambo kwa Ufanisi na Ubora ambayo ni:-

i. UFAHAMU(Cognizance), kuelewa maana ya kufanya jambo kwa UFANISI na UBORA. Hauwezi kuwa au kufanya kitu usichoelewa vizuri.

ii. TAFAKARI (Cogitate), Ukifikiri na kutafakari sana jambo, unaliumba ndani yako na ndilo linalotokea. Kile unachofikiri ndicho kinakujia. Ukifikiri na kutafakari Ufanisi na Ubora ndicho kitachofanyika kwako.

iii. KUJITOA(Commitment), Kuhakikisha unajitoa kwa moyo wako wote kufanya mambo kwa UFANISI na kwa UBORA. Usipojitoa utaishia kufanya mambo kwa kulipualipua.

iv. JITIE MOYO(Courage), Kujitia nguvu kwa kujiambia kwamba inawezekana kuwa BORA na inavutia kufanya mambo kwa UFANISI na UBORA. Jipe moyo binafsi.

v. ENDELEA KUFANYA (Consistence), ili jambo liwe tabia na kawaida yako, ni muhimu kujenga msingi wa kudumu kulifanya bila kuacha. Endelea kufanya kila jambo kwa UFANISI na UBORA.

vi. BOBEA(Competence); hakikisha unajua sana na una utaalamu wa kutosha kufanya mambo. Kubobea kunafanya urahisi katika kufanya mambo kwa UFANISI na UBORA.

vii. *UJASIRI*(*Confidence*); Amini katika uwezo na utaalamu ulionao. Hivi itakujengea ujasiri na utafanya jambo lolote kwa UFANISI na UBORA.

viii. *UMAKINI*(*Concentration*); Hakikisha fikra na akili yako yote unaiweka kwenye jambo unalolifanya, hii itakusaidia kufanya kwa UFANISI na UBORA.

ix. *LIPA GHARAMA*(*Costing*); Jambo lolote lenye UFANISI na Ubora linahitaji kugharamikiwa, uwe tayari kulipa gharama ya muda, nguvu, fedha, na kila kinachohitajika ili kufanya jambo kwa UFANISI na UBORA.

x. *JIDHIBITI*(*Composure*); hakikisha unajisimamia na kusimamia mambo yako ili kujipa nafasi ya kutochanganya mambo, hii itakusaidia kufanya mambo kwa UFANISI NA UBORA.

Mtu wa kiume anayefanya mambo kwa UFANISI na UBORA ni Mwanaume halisi. Mwanaume huwa haborongi mambo, anafanya kwa UFANISI na UBORA.

18. Ni USHINDANI!

*“Maana ingawa tunaenenda katika mwili,
hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; (Maana silaha za*

vita vyetu si silaha za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome” 2 Wakorintho 10:3,4

“Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho” Waefeso 6:12

Kila siku Mwanaume anapigana vita na majitu mbalimbali kwenye maisha yake. Ukiangalia katika Biblia unaona namna ambavyo katika nyakati mbalimbali Watoto wa kiume walitakiwa kuuwawa. Wakati wa kuzaliwa kwa Musa, Farao aliagiza Watoto wote wa kiume wauwawe, na wakati wa kuzaliwa kwa Yesu, Herode aliagiza Watoto wa kiume wauwawe.

Daima nuizo kubwa la mashambulizi na mikakati ya shetani ni kwa wanaume. Shetani anajua akimpiga mwanaume akamshinda, ameishinda jamii na hata Taifa. Ni muhimu utambue kwamba kila wakati shetani kama Simba angurumaye akimtafuta mtu ammeze. Na wanaume tupo vitani, ni muhimu kujipanga, kujihami na kupambana kwa akili.

Kimsingi zipo aina tano za vita anazopigana mwanaume kila wakati ambazo ni; -

- i. **VITA VYA KIROHO;** Ni aina ya vita vinavyopigana kwenye Ulimwengu wa Roho kwa njia ya Maombi. Na hii ndio maana ni muhimu mwanaume kuwa na nguvu za Rohoni kupitia Ibada ili kumshinda Adui. Hii ndio vita Kubwa kuliko zote.
- ii. **VITA YA KIUCHUMI;** Hii ni vita anayopigana mwanaume ya kujiondoa kwenye umaskini na ukata. Ni vita kwenye kazi za mikono anayofanya mwanaume. Ili kushinda ni lazima kujiunganisha na Uchumi na kiMungu.
- iii. **VITA YA KIMAADILI;** Hii ni vita anayopigana mwanaume juu ya kulinda maadili na ushuhuda wake. Ni vita ya kitabia ambayo Mwanaume anapambana ili kuwa mfano na kielelezo kwenye jamii na Taifa.
- iv. **VITA YA HATIMA;** Kila mwanaume anapambana kutengeneza hatima njema juu yake binafsi, familia, jamii na hata taifa. Anapambana na

kuimarisha baadae(future) yenye nguvu na inayoeleweka.

v. VITA YA KIFAMILIA; Hii ni vita inayohusisha ndoa, watoto na uzao wake kwa ujumla. Mara zote adui anataka kuambukiza/kurithisha kufeli au kushindwa kulikotokea kwenye uzao uliotokea utokee na kwenye uzao wako pia. Wanaume hupigana hii vita ili kujenga familia, uzao na kizazi imara chenye Mungu.

Mwanaume ni mtu wa Vita, ni mpambanaji, shujaa na mlinzi. Hakikisha daima unapambana kiume kwa kuwezeshwa na Mungu.

19. Ni UNAOMBATANA nao na UNAOJIFUNZA KWAO!

“Enenda pamoja na wenyе hekima, nawe utakuwa na hekima; Bali rafiki wa wapumbavu ataumia”
Mithali 13:20

“Usifanye urafiki na mtu mwenye hasira nyingi; wala usiende na mtu wa ghadhabu nyingi; usije ukajifunza njia zake; Na kujipatia nafsi yako mtego” Mithali 22:24,25

“Chuma hunoa Chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake” Mithali 27:17

Marafiki zako ni kina nani? Mara nyingi unaambatana na watu gani?. Ni watu gani unatamani kuwa kama wao (Role models)?, Ni nani ndio washauri na walezi wako?, Ni nani unapenda kusikiliza na kujifunza kwao?.

Nimeuliza hayo maswali kwa makusudi kabisa, Biblia inaweka wazi kabisa kwamba ukienda na wenyе hekima na wewe utakuwa na hekima. Lakini pia ukienda na wapumbavu na wewe utakuwa mpumbavu. Wewe ni matokeo ya marafiki na watu unaoambatana nao.

Wewe ni wastani wa watu watano unaotumia muda wako mwingi nao kila wakati. Mtu mmoja alisema “***Nionyeshe marafiki zako NA nitakuambia ulivyo***”. Na mwingine akasema “***Ndege wafananao huruka pamoja***”. Namna na jinsi ulivyo ni matokeo ya watu unaotembea nao.

Ukijiona haupo jinsi unavyotaka uwe, basi kwa urahisi zaidi BADILI AINA YA MARAFIKI ulionao. Tafuta aina ya marafiki wenyetabia, sifa na hulka kama unazotaka kuwa nazo kisha AMBATANA nao, Danieli aliambatana na Shedrack, Meshaki na Abednego kwa sababu walikuwa na sifa na tabia zilizolandana. Hakikisha urafiki wako unakuwa wa faida. Marafiki wanaweza kukusababishia KUFELI au KUFAULU kwako kwenye jambo lolote.

Lakini pia watu wengine ambao wana ushawishi mkubwa sana katika Maisha yetu ni washauri/walezi wetu. Hebu angalia Eliya alisababisha Elisha kufanikiwa, Musa alisababisha Yoshua kufanikiwa, lakin pia Paulo alisababisha Timotheo kufanikiwa. (Mentors) wana athari kubwa sana kwenye Maisha yetu, (Role Models) wana athari kubwa sana maishani mwetu.

Ni hekima kuwa na watu wa mbele yako waliofanikiwa kwenye Uanaume, yaani waliosimama vizuri kwenye Ndoa na familia zao. Ni Waume na Wababa wanaoeleweka. Kila wakati fahamu kwamba FAMILIA ndio kipaumbele, lakini pia ndio kipimo cha MWANAUME kufaulu au kufeli kwenye Uongozi.

Epuka kuambatana na watu wasio na mitazamo ya kiunaume, Epuka kuambatana na watu wanaochukulia poa(wepesi) na kudharau mambo ya kifamilia. Epuka kuambatana na watu wanaofikiri PESA, KAZI au HUDUMA ndio kila kitu. Kama mtoto wa kiume ni lazima ujifunze kupima na kujiridhisha kabla ya kujihusisha na mtu au kitu. Kumbuka watu wanakutambua kwa aina ya watu unaoambatana nao zaidi, marafiki na watu wanaokuvutia au wenyе ushawishi zaidi maishani mwako. Mungu akusaidie katika Jina la Yesu.

20. Ni KUDHIHIRISHA UBABA!

“Yusufu akamwangukia babaye usoni, akamlilia, akambusu ” Mwanzo 50:1

Mathayo 7:9-11” Au kuna mtu yupi kwenu ambaye mwanae akimwomba mkate, atampa jiwe?. Au akiomba samaki atampa nyoka?. Basi ikiwa ninyi mlion waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema. je! Si Zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa wao wamwombao?”

Mithali 4:10-12 “Mwanangu, sikiliza na kuzipokea kauli zangu; Na miaka ya Maisha yako itakuwa mingi. Nimekufundisha katika njia ya hekima; Nimekuongoza katika mapito ya unyofu. Uendapo, hatua zako hazitadhiikika, wala ukipiga mbio hutajikwaa.”

Licha ya kuwa na MABABA wengi duniani, UBABA unaelekea kutoweka kabisa. Na hii ni kwa sababu tuna MABABA jina wengi, na sio MABABA majukumu. Unajua nini, Neno BABA limetokana na neno la Kiebrania “ABBA” linalomaanisha MSINGI, CHANZO, MHIMILI, MPAJI, MWEZESHAJI na pia MLINZI. Na kwa hivyo basi haupaswi kuitwa BABA halafu usiwe chanzo, msingi, mhimili,

mwezeshaji, mlinzi na mpaji wa familia yako yaani mke na watoto.

Nilisema pale mwanzoni kwamba leo tuna MABABA jina wengi wasiotimiza majukumu ya UBABA hata kidogo. Hili limenisukuma kukuandika aina saba za MABABA nilizojifunza miaka mingi iliyopita kupitia mafundisho ya Televisheni. Ukumbuke tu kwamba kila aliyezaliwa wa kiume alitarajiwa kuwa BABA na asimame kwenye nafasi yake ya UBABA.

AINA ZA MABABA

i. Sperm Donor Dad (Mgawa mbegu za kiume), Baba mwenye lugha laini, asiyejituma, anapenda sana tendo la ndoa, anasababisha mimba halafu anasepa kinachotokea hakimuhusu.

ii. Provisional Dad (Baba mtoaji), Anatoa mahitaji yote ya familia, ila hana muda na familia wala hataki kujua kinachoendelea kwa mke na Watoto.

iii. Empty Promise Dad (Baba ahadi hewa) Huyu ni bingwa wa kutoa ahadi kwa mke na watoto,

asiyetimiza hata moja, ameja uongo na uzembe usio wa kawaida.

iv. Staff Dad (Baba Kazi) huyu ni baba anayetoa mahitaji kwa familia, asiye na muda na familia, kila wakati yupo bize na kazi na mambo ya ofisi. Hajui chochote kuhusu Watoto.

v. Mad Dad (Baba mwehu) huyu ni baba wa hasira na kelele kila wakati, daima hukemea Na kuwabughudhi watoto, hukosoa kila kitu. Hana muda wa kuwasifia wala kuwatia moyo watoto. Huonekana kama kituo cha polisi kwa Watoto wake.

vi. Step Dad (Baba wa kambo) baba wa aina hii huwa wa aina mbili, wapo wale wabaya ambao huwachukia na kuwachukulia vibaya hawa watoto kwa kuwa sio wake. Na wapo wasioongelewa sana, Ni baba wa kambo lakini huwalea watoto vizuri sana kama wake bila ubaguzi.

7. *Real Dad* (Baba wa Ukweli/Bora) Huyu ni baba anayesimama kwenye nafasi yake ipasavyo. Hutoa Mahitaji yote ya familia, hulinda na kutunza familia,

hupata muda maalum kwa ajili Ya mke na Watoto. Hujifunza Neno na Kuomba pamoja na familia. Kwa kifupi ni baba Anayejitambua.

Tukumbuke sisi kama wanaume ndio mfano na utukufu wa Mungu, Mungu ni Baba wa Milele. Daima amesimama kwenye nafasi kama baba inavyotakiwa, na sisi tulio wa mfano wake ni lazima na muhimu tusimame kwenye nafasi zetu za UBABA kama inavyotakiwa.

Kwa Toleo hili, nimeishia hapa. Ila Kaka yenu nitarudi tena kwa ajili yenu enyi Wavulana wa Tanzania.